# Unyambulishaji na Dhana ya Uelekezi katika Lugha ya Kikuria

*Mary Z. Charwi*

**Ikisiri**

Mofolojia ya vitenzi ni uwanja muhimu katika lugha yoyote ile duniani kutokana na ukweli kuwa kila lugha ina vitenzi na tabia ya vitenzi hutofautiana kutoka lugha moja hadi nyingine. Vitenzi vya lugha za Kibantu vina sifa ya kuambikwa viambishi awali na viambishi tamati. Mojawapo ya viambishi tamati ni viambishi vya kauli mbalimbali. Viambishi hivi huweza kuathiri muundo wa kitenzi ama muundo wa tungo kwa ujumla katika kuleta maana inayohusika. Mfano, kitenzi elekezi huweza kuwa si elekezi, si elekezi huweza kuwa elekezi ama kitenzi elekezi kuhitaji yambwa nyingine. Makala haya yanalenga kuelezea matokeo ya vitenzi vya Kikuria baada ya unyambulishaji na idadi ya viambishi vinavyoweza kuwekwa pamoja kwenye kitenzi.

## 1.0 Utangulizi

Kama ambavyo imeoneshwa katika kazi mbalimbali zilizotangulia, lugha za Kibantu zina utajiri mkubwa sana wa unyambulishaji wa vitenzi wenye umuhimu wa kisintaksia (Rugemalira, 1993; Khamis, 2008). Makala haya yanachunguza kwa undani kauli tano zalishi katika lugha ya Kikuria[1].

Massamba (2004) anaelezea unyambulishaji kama utaratibu wa kupachika viambishi kwenye mizizi ili kuunda maneno mapya. Kulingana na TUKI (2004) unyambulishaji ni uambatishaji wa viambishi kwenye mzizi ili kujenga neno jipya. Ngonyani (2003) hatofautiani na waandishi hawa kuwa unyambulishaji wa vitenzi kama mchakato wa uundaji wa maneno husababisha uundaji wa kitenzi kipya chenye maana panuzi. Hivyo basi kupitia mchakato huu lugha hujiongezea maneno zaidi yanayotumiwa katika kuwasilisha maana fulani kisemantiki na hivyo kuleta mabadiliko ya kisintaksia. Eastman (1967) anasisitiza kuwa kiundani tunaona kuwa uambishi huu huweza kubadili maana ya neno ama kubadili aina ya neno kutoka kwenye kategoria moja kwenda nyingine.

Lugha nyingi za Kibantu, kama sio zote, zina idadi kubwa ya viambishi vinyambulishi ambavyo vinaweza kuleta tofauti ya maana na kazi ya kitenzi. Hapo awali wazo hili liliungwa mkono na Guthrie (1970) na Rugemalira (1993) kwa kusisitiza kuwa unyambulishaji unapanua mzizi wa kitenzi cha Kibantu sio tu kimofolojia bali pia kisemantiki. Hii pia inaelezwa na Lodhi (2002) kuwa unyambulishaji wa vitenzi ni zaidi ya dhana ya unyambulishaji bali inahusisha viambishi vyote kabla ya kiambishi tamati. Wataalamu wengine wameonesha kuwa unyambulishaji wa vitenzi una matumizi pekee hasa katika muktadha wa

[1] Kikuria ni mojawapo ya lugha za Kibantu katika koo ya Mashariki ya Niger-Congo kundi namba (E43) kwa mujibu wa Guthrie (1967). Tanzania lugha hii imepakana na lugha ya Kizanaki (E44), Kinata (E45), na Kisimbiti (JE431), wakati Kenya imepakana na lugha ya Kilogoli (E41) na Kikisii (E42).

uhusika katika sentensi fulani (taz. Khamis, 2008). Hivyo basi, makala haya yanachanganua unyambulishaji wa vitenzi vya Kikuria ili kuonesha dhana ya uelekezi inavyojitokeza, kama Rugemalira (1993) anavyochambua katika Kinyambo. Pia uchambuzi huu una lengo la kuonesha upekee na ufanano wa lugha hii na lugha nyingine za Kibantu, kama zinavyoelezwa na waandishi mbalimbali.

Utafiti huu ulifanywa kwenye jamii ya Kikuria mwaka 2010 katika Mkoa wa Mara wilaya ya Tarime katika vijiji vinne: Rosana, Nyamwigura, Borega na Mogabiri. Mtafiti alitumia mbinu ya mahojiano, dodoso na majadilianao katika makundi. Uchaguzi wa wahojiwa ulikuwa wa makusudi yenye kulenga watu ambao wangeweza kujibu maswali ya mtafiti. Idadi ya wahojiwa ilikuwa kumi na sita katika vijiji hivyo vinne.

## 2.0 Mapitio ya Maandishi kuhusu Unyambulishaji wa Vitenzi vya Kibantu

Unyambulishaji wa vitenzi ni dhana ambayo imefanyiwa utafiti na wataalamu mbalimbali katika lugha mbalimbali za Kibantu. Miongoni mwa tafiti hizo ni Kinyambo (Rugemalira, 1993), Kiswahili na Kinyamwezi (Lodhi, 2002), Kibosho (Mushi, 2005), Kisukuma-Jinakiiya (Muhdhar, 2006), Giha (Ezekiel, 2007), Chindali (Masebo, 2007), Kiswahili (Moore, 1966 na Khamis, 2008) na Kikuria (Zacharia, 2011).

Pia tunaona kuwa ijapokuwa unyambulishaji unaonekana kufanana katika lugha nyingi za Kibantu, bado kuna upekee wa lugha moja na nyingine. Mfano, Rugemalira (1993), Lodhi (2002), Mushi (2005), Khamis (2008), Kaoneka (2009) na Zacharia (2011) wanadhihirisha upekee wa lugha hizo. Katika malengo mahususi ya makala haya tutajikita zaidi kwenye athari za unyambulishaji kisintaksia na idadi ya viambishi vinavyoweza kuwekwa pamoja katika kitenzi.

Lodhi (2002) analinganisha unyambulishaji wa vitenzi katika lugha ya Kiswahili na ya Kinyamwezi. Anagundua kuwa baadhi ya vitenzi vikiwekewa viambishi vya utendea husababisha unyume / kinyume cha upande wa pili, kama inavyojidhihirisha katika mfano ufuatao.

(1) a. nuka nuk-i-a
b. hama ham-i-a

Pia katika utafiti wake hakueleza kuwa vitenzi hivi vinaweza kubeba viambishi nyambulishi vingapi kwa wakati mmoja na nini athari zake kisintaksia. Maarifa haya yangeweza kuongeza ujuzi na uelewa katika uwanja huu wa Isimu.

Mushi (2005) anabaini kuwa kiambishi cha utendwa ni - *o* - huwekwa mwishoni mwa kitenzi, na anaeleza kuwa vitenzi vingine katika lugha ya Kibosho viko katika utendwa lakini maana zake ni za utenda. Kwa upande wake, Kaoneka (2009:83-87) anaeleza kuwa katika lugha ya Kishambala unyambulishaji hubadili mofolojia ya kitenzi ambacho huwa na athari kisintaksia na kisemantiki. Mwandishi anasisitiza kuwa ingawa unyambulishaji wa vitenzi katika lugha ya Kishambala unafanana na wa lugha nyingine za Kibantu, lugha hii ina upekee wake ambao unaitofautisha na lugha nyingine. Kwanza kabisa, vitenzi vyake huweza kuambikwa viambishi nyambulishi vitatu hadi vinne, tofauti na lugha nyingine kama vile Kinyambo, Rugemalira (1993), Chasu na Kikongo. Angalia mifano hii hapa chini toka kwa Kaoneka na Rugemalira:

Kaoneka (2009:83-87).

(2) (52) wana wa- za- boh- **e-z** **e-** **an-** a makui
the children SM- PST- bark- CAUS-APPL- REC- FV dogs
'the children caused the dogs to bark against each other'.

(3) (53) waghoshi wa- za- ish- **i-** **iz-** **an-** a ngoto
the men SM- PST- graze- APPL-CAUS-REC-FV sheep
'the men made the sheep to graze for each other'.

(4) (56) a) wavyee wa-za- mem- **ez-** **esh-** **e-** **an-** a ngahu
the women SM- PST- full- CAUS-INT- APPL- REC-FV baskets
'the women made each other's basket completely full'.

b) waishi wa- za- ighut- **ish-** **iz-** **i** **-** **an** **-** a ngoto
herders SM- PST- satiate- INT- CAUS-APPL- REC- FV ngoto
'herders made each other's sheep over satiated'.

Angalia mifano hii kutoka kwenye Kinyambo, Rugemalira (1993:188):

(5) (607) a - ka - ji- kom -er-w- a Kakúru
she-PST - it- tie -A -P-FV Kakúru
'she was tied it for by Kakúru'

(6) (608) a - ka- mu- kor - ez-á egáari (ez <- er-¡-)
she-PST-him-repair-A+C-FV bicycle
'she had the bicycle repaired for him'

Pili, Kishambala kinaruhusu mfuatano huru wa viambishi nyambulishi vya utendea na utendano (Applicative and reciprocal) tofauti na lugha nyingine ambazo hufuata nadharia ya Hyman (2003) inayosisitiza kuwa viambishi

vinyumbulishi ni lazima vifuate mfuatano wa CARP[2] (Kaoneka, 2009:100). Hii inathibitisha mwachano na upekee katika lugha za Kibantu.

Kauli za utendea, utendeshi, utendano, utendwa na utendeka zimeonekana kuwa zalishi tofauti na kauli zingine kama inavyoelezwa na waandishi mbalimbali mfano (Rugemalira, 1993), (Lodhi, 2002), (Mushi, 2005), (Muhdhar, 2006), (Ezekiel, 2007), (Masebo, 2007), (Moore, 1966 na Khamis, 2008) na (Zacharia 2011). Kwa mfano, Rugemalira (1993) katika utafiti wake kwenye lugha ya Kinyambo ameshughulikia viambishi vya *utendea, usababishi, utendano, utendwa na utendeka* na amebaini kuwa viambishi hivi vina uwezo mkubwa wa uzalishaji. Rugemalira ameonesha idadi ya juu ya viambishi vinavyoweza kuwekwa pamoja katika kitenzi kuwa ni tatu na athari yake kisintaksia inategemea ni kiambishi gani kimewekwa kwenye kitenzi. Utafiti wake unaonesha kuwa viambishi vya kauli mbalimbali huweza kubadili aina moja ya kitenzi kwenda aina nyingine kisintaksia.

Halikadhalika, Khamis (2008), anazungumzia namna unyambulishaji wa vitenzi katika Kiswahili unavyoathiri viambishi yambwa na viambishi vyenyewe katika lugha hiyo. Mtaalamu huyu anajadili unyambulishaji unaofanana na ule wa Rugemalira (1993) hasa katika kuelezea namna unyambulishaji husika unavyoathiri wahusika (yambwa) katika sentensi.

Ingawaje Lodhi (2002:24) analinganisha unyambulishaji katika lugha ya Kiswahili na Kinyamwezi anahitimisha kwa kusema kuwa, unyambulishaji wa lugha hizi unafanana. Hata hivyo ulinganishaji wa Lodhi katika lugha hizi haukueleza ni namna gani viambishi vinyambulishi vinavyoweza kuwekwa pamoja na athari yake kisintaksia, hii inajidhihirisha hapa kama anavyosema:

> "The present paper investigates "verbal extensions" as a morphological and not a semantic category, though I believe the question of verb derivation in Bantu needs to be addressed as syntactic and semantic categories".

Hivyo basi kwa mantiki hii makala haya yanachunguza na kufafanua athari za unyambulishaji kisintaksia hususan katika dhana ya uelekezi katika lugha ya Kikuria.

---

[2] CARP: C- Causative (usababishi), A- Applicative (utendea), R- Reciprocal (utendano), na P- Passive- (utendwa). SM-subject maker, PST-Past, INT- Intensive, CAUS-Causative, APPL- Applicative,REC- Reciprocal, FV-Final vowel.

Kwa kifupi, vitenzi vya Kibantu vinaweza kugawanywa katika makundi tofauti tofauti kwa kutumia kigezo cha kisemantiki au kisintaksia. Kwa mfano, kisemantiki kuna vitenzi vinavyoelezea tendo katika hali fulani mfano kujua, kuwa, n.k. Vitenzi vinavyoelezea mwendo kwa mfano, kimbia, tembea, n.k. vya matendo kama vunja, kata, n.k. Kisintaksia, vitenzi hugawanywa kwa kuzingatia uhitaji wa wahusika katika kukamilisha tendo hilo. Kwa mfano kuna vitenzi vinavyohitaji mhusika mmoja tu yaani mtenda (intransitive verbs) ‘mtoto amelala’, ‘mbwa amekufa’; vinavyohitaji wahusika wawili (transitive verbs) ‘baba amenunua gari’, ‘Juma amechukua kikombe’; vinavyohitaji wahusika / vihusika wa/vitatu (ditransitive verbs), ‘Mwalimu amempa mwanafunzi daftari’, ‘kaka ameweka kitabu mezani’, n.k.

Makala haya yanelenga kuonesha athari ya unyambulishaji kisintaksia, hususan dhana ya uelekezi. Hii inabainisha kuwa dhana ya unyambulishaiji haiishii tu kuongeza neno jipya bali kupanua maana kisemantiki na kisintaksia. Pia tutaona kuwa kuna uwiano kati ya aina za vitenzi vya Kibantu na aina ya yambwa zinazotakiwa kuambatana na vitenzi hivyo katika sentensi. Mreta (1998) ameonesha aina mbalimbali za vitenzi vya Kibantu na makala haya yataweza kuonesha jinsi unyambulishaji unavyotegemea aina ya vitenzi. Pia makala haya yataonesha namna unyambulishaji unavyoathiri yambwa katika Kikuria.

**3.0 Viambishi Nyambulishi vya Asili**

Kutokana na mapitio mbalimbali, baadhi ya lugha za Kibantu zimeendelea kubaki na viambishi vinyambulishi vya asili, wakati katika lugha nyingine viambishi hivi vimepitia michakato mbalimbali (mofofonemiki) na kupata sura mpya. Vifuatavyo ni viambishi vinyambulishi asilia kulingana na waandishi Schadeberg (2003), Guthrie (1970) na Meinhof (1932):

**I. Viambishi nyambulishi vya asili vya kauli tano katika lugha za Kibantu**

| **Na.** | **Kauli** | **Viambishi** | | |
|---|---|---|---|---|
| | | **Schadeberg** | **Guthrie** | **Meinhof** |
| 1 | Applicative - utendea | *-ɪl- | cf. Directive | *{-da} |
| 2 | Causative - usababishi | *-i-/- ici- | *iic/ | *{-ya} |
| 3 | Passive - utendwa | *-u-/-ibu- | *u / bu | *{-wa} |
| 4 | Reciprocal - utendano | *-an- | *an | *{na} |
| 5 | Stative - utendeka | *-am- | *am/(*ɪk) | ------------ |

Viambishi nyambulishi vya Kikuria havitofautiani sana na viambishi asilia vilivyooneshwa na Schadeberg (2003) isipokuwa baadhi ya sauti chache kama inavyojidhihirisha hapa chini. Hii ni kutokana na michakato mbalimbali ya kimofofonolojia ya mabadiliko ya sauti toka sauti moja kwenda nyingine. Mabadiliko haya husababisha kudhoofika au kuimarika kwa sauti iliyobadilika.

**II. Viambishi nyambulishi vya asili na vya Kikuria**

| **Na.** | **Kauli** | **Viambishi** | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | **Schadeberg** | **Guthrie** | **Meinhof** | **Kikuria** |
| 1 | Applicative-utendea | *-ɪl- | cf. Directive | *{-da} | -er- / ir |
| 2 | Causative-usababishi | *-i-/- ici- | *iic/ | *{-ya} | -i- / -isi- |
| 3 | Passive - utendwa | *-u-/-ibu- | *u / bu | *{-wa} | -w- / -bhw- |
| 4 | Reciprocal-utendano | *-an- | *an | *{na} | -an- |
| 5 | Stative - utendeka | *-am- | *am/(*ɪk) | ----------- | -ek- / -ik- |

Makala haya yameshughulikia kauli zalishi tano ambazo ni: *utendea*, *usababishi*, *utendano*, *utendwa* na *utendeka*. Angalia mifano hapa chini ya viambishi vya kauli hizi kama zinavyoweza kujidhihirisha katika lugha hii:

**III. Viambishi nyambulishi vya kauli tano katika lugha ya Kikuria**

| **Kauli** | Utendea (utd) | Usababishi (usb) | Utendano (utn) | Utendwa (utw) | Utendeka (utk) |
|---|---|---|---|---|---|
| **Viambishi** | *-er-/-ir-* | *-i- , -isi-* | *-an-* | *-w-, -bhw-* | *-ek- / -ik-* |
| **Mfano**: bhuna | *bhon-er-a* | *bhun-i-a* | *bhun-an-a* | *bhun-w-a* | *bhon-ek-a* |
| **Tafsiri**: vunja | vunjia | vunjisha | vunjana | vunjwa | vunjika |

### 3.1 Athari za Kauli mbalimbali Kisintaksia

Vitenzi vya Kikuria kama ilivyo kwenye lugha nyingi za Kibantu huwa na sifa tofautitofauti kulingana na aina ya kitenzi. Kwa mfano vitenzi si elekezi havihitaji yambwa wakati vitenzi elekezi huhitaji yambwa moja au mbili kulingana na asili ya kitenzi chenyewe. Athari za vitenzi hivi hutofautiana kutokana na aina za viambishi vilivyopachikwa kwenye mizizi ya vitenzi hivyo.

### 3.2 Kauli ya Utendea na Usababishi[3]

Sehemu hii tunajikita kwenye aina za vitenzi si elekezi na elekezi, vinavyoathiriwa na unyambulishaji katika kuleteleza yambwa. Utendea na usababishi ni kauli zinazoonekana kuwa na uzalishaji wa kiwango cha juu katika lugha hii ya Kikuria. Kwa mfano, katika vitenzi 81 tulivyokusanya vitenzi 78 vinakubali kuambikwa viambishi hivi na vitenzi vitatu vinakataa. Uzalishaji unaofafanuliwa hapa ni uwezo mkubwa wa kukubali kuambikwa katika vitenzi vingi.

#### 3.2.1 Kauli ya Utendea

Kuna mkanganyiko kati ya mofu na mofimu katika lugha za Kibantu. Makala haya yatatumia dhana ya mofu ikiwa na maana ya sehemu halisi ya neno inayobeba maana (mofimu), wakati mofimu ni dhana dhahania iliyoko akilini mwa mtu ibebwayo na mofu. Mofu ya kauli ya utendea katika lugha ya Kikuria ni -*er*- au -*ir*-, na ikipachikwa kwenye mzizi wa kitenzi husababisha athari za kisintaksia. Tazama mifano ifuatayo:

(7). *omoona arakúúra*
mtoto analia (kt.[4] si elekezi)

(8). *omoona a - ra - kóór - er - a eghekebhi*
mtoto kba - nj - mz - utd - kbt
mtoto analilia kisu (kt. elekezi)

(9). *tata arakúa*
baba anakufa (kt. si elekezi)

(10). *tata a - ra - kú - er - a komoro*
baba kba - nj - mz - utd - kbt mtoni
baba anafia mtoni (kt. elekezi)

(11). *bhabha aratema omoona*
mama anampiga mtoto (kt. elekezi)

(12). *bhabha a - ra - tem - er - a omoona ing'imbo*

---

[3] Wanaisimu mbalimbali wanatumia msamiati tofauti katika kuzungumzia dhana hizi. Kwa mfano, unyambulishaji fanyizi (Khamis, 2008: 62) unaitwa kiambishi kitendeshi (Kihore na wenzie 2003: 126) au kauli sababishi. Makala haya hayajikiti katika upande wowote bali yanatumia msamiati unavyojitokeza.

[4] Vifupisho hivi vimetumika kama ifuatavyo kt- kitenzi, kba- kiambishi awali, nj-njeo, mz-mzizi, utd-utendea, utn-utendano, usb-usababishi, utw-utendwa, utk-utendeka, na kbt-kiambishi tamati

mama kba - nj - mz - utd - kbt mtoto fimbo
mama anampigia mtoto fimbo (kt. elekezi)

(13). *tata araha omoona ichimbiria*
baba anampa mtoto fedha (kt. elekezi)

(14). *tata a - ra - h - er - a omoona ichimbiria irungu*
baba kba - nj -mz - utd - kbt mtoto fedha chumbani
baba anampea mtoto fedha chumbani (kt. elekezi)

Kama inavyojionesha hapo juu, katika mifano (7-9) kauli ya utendea husababisha kitenzi si elekezi kuwa elekezi na katika mifano (10-14) kitenzi elekezi kuhitaji yambwa ama kipashio kingine katika kukidhi dhima za dhamira mabalimbali kulingana na uhitaji wake. Pia katika mfano wa 12 na 14 mofu -*er*- imelazimisha kuwapo kwa vipashio *ing'imbo* 'fimbo' na *irungu* 'chumbani' kama vipashio vya lazima.

### 3.2.2 Kauli ya Usababishi

Kauli hii katika lugha ya Kikuria ina mofu mbili yaani -*i*-, na -*isi*-. Mofu -*i*- inaonekana kukubalika kwenye vitenzi vingi zaidi kuliko -*isi*-. Tazama mifano ifuatayo:

(15) *omoona a - ra - ghw - a*
mtoto kba - nj - mz - kbt
mtoto anaanguka (kt. si elekezi)

(16) *Mwita a - ra - ghw - isi - a omoona*
Mwita kba - nj - mz - usb - kbt mtoto
Mwita anaangusha mtoto (kt. elekezi)

(17) *abhaana bha - ra - tuk - a amasimo*
watoto kba - nj - mz - kbt mashimo
watoto wanachimba mashimo (kt. elekezi)

(18) *Marwa a - ra - tuk- i - a abhaana amasimo*
Marwa kba - nj - mz - usb - kbt watoto mashimo
Marwa anawachimbisha watoto mashimo *(*kt. elekezi)

Athari inayopatikana hapa ni kuongezeka kwa mtenda mpya (msababishi) na mtenda wa awali wa jambo anahamia upande wa yambwa lakini anabaki na sifa yake ya (utenzi) kutendeshwa. Kitenzi kilichokuwa si elekezi mfano (15)

*araghwa* ‘anaanguka’ kinapata sifa ya kuwa kitenzi elekezi (16) *araghwisia* ‘anaangusha’. Kauli hii inakiongezea kitenzi kipashio kimoja ambacho ni mtendaji mpya au msababishi. Kiambishi *-i-* cha kauli ya usababishi kimeonekana kuwa kizalishi kwa kiasi kubwa kuliko kiambishi -isi- ambacho kinaonekana kupotea na kuweza kutumika kwa vitenzi vichache sana. Mifano ifuatayo hapa chini kwenye jedwali inadhihirisha haya.

**III. Viambishi Sababishi *-i-* na *-isi-***

| Kitenzi-Kisw | Kitenzi-Kikuria | *-i-* | *-isi-* | maana |
|---|---|---|---|---|
| lima | *rem-a* | *rim-i-a* | - | limisha |
| nenepa | *nór-a* | *núr-i-a* | - | nenepesha |
| imba | *bhín-a* | *bhín-i-a* | - | imbisha |
| sema | *ghámb-a* | *ghámb-i-a* | - | semesha |
| tembea | *ghεεnd-a* | *ghεεnd-i-a* | - | tembeza |
| anguka | *ghw-a* | - | *ghw-isi-a* | angusha |

### 3.3 Kauli ya Utendano, Utendwa na Utendeka
Sehemu hii inashughulikia zaidi sifa ya yambwa pamoja na unyambulishaji unaotakiwa katika Kikuria hasa tukizingatia utendano, utendwa na utendeka. Kauli hizi, tofauti na usababishi na utendea, hukiondolea kitenzi hadhi ya kuhitaji yambwa na wakati huohuo huleta mabadiliko ya dhima baina ya vipashio vya sentensi. Pia hukifanya kitenzi kiwe na uhiari wa kuwekewa baadhi ya vipashio au kutokuwekwa.

#### 3.3.1 Kauli ya Utendano
Kisintaksia kauli hii inaondoa yambwa kutoka nafasi yake na kuihamishia kwenye kiima/ mtenda na wote yambwa na mtenda kupewa dhima mbili kwa wakati mmoja, yaani mtenda na wakati huohuo huwa mtendwa. Mfano:

(19) *Nyagige a - hanch - a mokae*
Nyagige kba - mz - kbt mkewe
Nyagige anampenda mkewe (kt. elekezi)

(20) *Nyagige na mokae bha - hanch - an - a*
Nyagige na mkewe kba - mz - utn - kbt
Nyagige na mkewe wanapendana (kt. si elekezi)

Kuongezeka kwa kauli hii hukipotezea kitenzi sifa ya kuhitaji yambwa na pia huleta mabadiliko ya nafasi ya kategoria moja (*yambwa*), pia mtenda wa awali na mtendwa hupewa dhima sawa, yaani ya kutenda na kutendwa kwa wakati mmoja.

### 3.3.2 Kauli ya Utendwa

Katika lugha ya Kikuria kauli hii huleta mabadiliko ya kisintaksia; kwanza, kwa kubadilishana nafasi kati ya mtenda na mtendwa na kipashio kimoja '*na*' huongezeka. Wakati mwingine sio lazima kuwapo kwa mtenda bali yambwa huchukua nafasi ya mtenda huku ikiendelea kubaki na dhima yake ileile ya mtendwa. Mfano:

(21)a *abhaana bha - ra - rút - a urusiri*
watoto kba - nj - mz - kbt kamba
watoto wanavuta kamba (kt. elekezi)

b. *urusiri ru - ra - rút - w - a na abhana*
kamba kba - nj - mz - utw- kbt
kamba inavutwa na watoto (kt. si elekezi)

c. *urusiri ru - ra - rút - w - a*
kamba kng 11- nj - mz - utw- kbt
kamba inavutwa (kt. si elekezi)

(22) a. *omoghaka a - ra - táki - a omoona*
mzee kba - nj - mz - kbt mtoto
mzee anamshtua mtoto (kt. elekezi)

b. *omoona a - táki - bhw - i*
mtoto kba - mz - utw - kbt
mtoto ameshtuliwa. (kt. si elekezi)

(23) a. *omoona a - ra - tírí - a eghekebhi*
mtoto kba - nj - mz - kbt kisu
mtoto ananoa kisu (kt. elekezi)

b. *eghekebhi ke - ra - tírí- bhw - a*
kisu kba - nj - mz - utw- kbt
kisu kinanolewa

c. *omoona a - ra - rughi - a esese*
mtoto kba - nj - mz - kbt mbwa
mtoto anamfukuza mbwa (kt. elekezi)

d. *esese e - ra - rughi - bhw - a*
mbwa kba - nj - mz - utw - kbt

mbwa anafukuzwa (kt. si lekezi)

e. *tata a - ra - righi - a ilichembe*
baba kba - nj - mz - kbt jembe
baba anatafuta jembe (kt. elekezi)

f. ilichembe *re - ra - righi - bhw - a*
jembe kba - nj - mz - utw - kbt
jembe linatafutwa (kt. si elekezi)

Kwenye mfano (21)a *abhaana* 'watoto' na *urusiri* 'kamba' ni vya lazima lakini kwenye (21)b mtenda *abhaana* si lazima kuwapo na hii haipotezi maana kama inavyojionesha katika (21)c, kwa sababu si kiambishi cha lazima. Kutokana na kutokuwa lazima, viambishi hivi vinapata sifa ya kupunguza kipashio kimoja, ambacho ni mtenda kwa sababu msisitizo uko kwenye yambwa. Kwa upande mwingine, kupachika kauli ya utendwa kumesababisha mabadiliko ya nafasi ya yambwa kuwekwa kwenye nafasi ya mtenda lakini ikibaki na hadhi yake ileile ya mtendwa. Hali hii hukifanya kitenzi elekezi kuwa si elekezi kama inavyojidhihirisha katika 22a - 23f. Kiambishi cha utendwa - *bhw* - hupachikwa kwenye vitenzi vyenye mizizi inayoishia na - *i* - , angalia mfano 22b, 23b, 23d na 23f hapo juu.

### 3.3.3 Kauli ya Utendeka

Kiambishi cha kauli ya utendeka katika lugha hii ni *-ek-*. Kauli hii hukiondolea kitenzi sifa ya kuwa elekezi na kukifanya kitenzi si elekezi.

(24) *omoona a - ra - bhún - a omote*
mtoto kba - nj - mz - kbt mti
mtoto anavunja mti

(25) *omote gho - bhón - ek - le*
mti kba - mz - utk - kbt
mti umevunjika

Kauli hii inakiondolea kitenzi sifa ya kuhitaji mtenda ambaye kisarufi ni mtendaji wa jambo na nafasi hii huchukuliwa na yambwa. Kama inavyooneshwa hapo juu (25) athari ya kauli hii hubadili kitenzi elekezi na kuwa kitenzi si elekezi. Hii ni kutokana na yambwa kuhamia kwenye nafasi ya mtenda, ambaye sasa hahitajiki tena. Hii ni athari kisintaksia kwa kuwa inapunguza kipashio kimoja kilichokuwapo awali na kukifanya kisihitajike tena.

**4.0 Muunganiko wa Kauli**

Sifa mojawapo ya vitenzi vya Kibantu ni kuweza kupachikwa viambishi zaidi ya kimoja kwa wakati mmoja kwa mzizi mmoja. Katika lugha ya Kikuria viambishi nyumbulishi vyaweza kupachikwa zaidi ya kimoja hadi vinne na kwa kujirudia baadhi ya viambishi huweza kuambikwa hadi vitano katika mzizi mmoja, kama inavyojidhihirisha hapa chini kwenye vipengele vinavyofuata.

**4.1 Muunganiko wa Kauli mbili katika Kitenzi kimoja**

Baada ya kuangalia aina tano za unyambulishaji katika Kikuria, sehemu hii inawasilisha jinsi Kikuria kinavyotumia unyambulishaji katika kuzalisha aina mbalimbali za uhusika. Pia sehemu hii ya makala haya itaonesha namna ambavyo mwambatano wa vipashio katika lugha za Kibantu (Hyman, 2003) unavyojitokeza katika lugha hii. Kwa kifupi, lugha hii ni mojawapo ya lugha za Kibantu inayoweza kuchukua viambishi vingi kwa wakati mmoja. Tukianza na kauli mbili:

**4.1.1 Kauli ya Usababishi na Utendano / Utendano na Usababishi**

Viambishi vya kauli hizi huweza kuambikwa kwenye vitenzi kwa wakati mmoja, na kwa kubadilishana nafasi huweza kuathiri kitenzi kama ifuatavyo:

(26). *Mwita a - ra - ghw - ísí - a Robhi*
Mwita kba - nj - mz - usb - kbt Rhobi
Mwita anamwangusha Robhi

(27). *Mwita na Robhi bha - ra - ghw - ísí - an - a*
Mwita and Robi kba - nj - mz - usb - utn - kbt
Mwita na Robhi wanaangushana

28. *abharisya bha - ra - ambuk - í - an - a omoro*
wavulana kba - nj - mz - usb -utn - kbt mto
wavulana wanavushana mto

Kiambishi cha usababishi kwenye mfano 26 kimebadili kitenzi si elekezi kuwa kitenzi elekezi kwa kuongeza msababishi / mtendeshi na mtendaji wa awali anageuzwa kuwa yambwa/ mwathirika wa tendo. Wakati utendano kwenye namba 27 umekiondolea kitenzi kipashio kimoja kwa kuunda kiima jumuishi. Jambo lingine la msingi katika lugha hii tofauti na lugha zingine za Kibantu ni kwamba, mfuatano wa viambishi vya usababishi na utendea huweza kuwa na mbadilishano huru bila kuathiri maana ya awali. Katika lugha zingine za Kibantu mfano Chichewa (taz. Hyman, 2003), ambapo mfuatano kama huu unaleta maana tofauti. Mifano ifuatayo inathibitisha yanayoelezwa hapa.

(29)a. *Mwita a - ra - hanch - an - i - a abhaana*
Mwita kba - nj - mz - utn - usb - kbt watoto
Mwita anawapendanisha watoto

b. *Mwita a - ra - hanch - i - an - a abhaana*
Mwita kba - nj - mz - usb - utn - kbt watoto
Mwita anawapendanisha watoto

(30)a *omoona na umukungu bha - ra - tuk - an - i - a amasimo*
Mtoto na mama kba - nj - mz -utn - usb - kbt mashimo
Watoto na mama wanachimbishana mashimo

b. *omoona na umukungu bha - ra - tuk - i - an - a amasimo*
Mtoto na mama kba - nj - mz - usb - utn - kbt mashimo
Watoto na mama wanachimbishana mashimo

(31) a. *Ghati na Robhi bha - ra - kiny - an - i - a*
Ghati na Robhi kba - nj - mz - utn - usb - kbt
Ghati na Robhi wanakimbizana

b. *Ghati na Robhi bha - ra - kiny - i - an - a*
Ghati na Robhi kba - nj - mz - usb - utn - kbt
Ghati na Robhi wanakimbizana

Kauli hizi zina athari tofauti kwani zinapowekwa pamoja kila moja hufanya kazi yake. Utendea huongeza kipashio kimoja na wakati huohuo utendano huathiri kipashio hicho kwa kukihamishia kwenye kiima na tunapata (kiima jumuishi). Hapa kiima hiki kina hadhi ya kutenda na wakati huohuo kuwa mtendwa. Katika muunganiko wa *utendano* na *usababishi*, baadhi ya vitenzi huruhusu mfuatano huru wa viambishi nyambulishi bila ya kuathiri maana. Lakini hii ifahamike kuwa huu mfuatano huru usiobadili maana ni kwa kauli hizi mbili na siyo zote.

### 4.1.2 Kauli ya Utendea na Utendano

Kauli zingine ambazo zaweza kukaa pamoja ni utendea na utendano. Muungano wa kauli hizi hukubalika katika lugha hii kama inavyojidhihirisha hapa chini mfano (32-35). Kauli hizi zinaruhusu pia mfuatano huru tofauti yake ni kuwa huathiri maana.

(32). *Robhi arahinya omote*
Robhi anainamisha mti

(33). *Robhi a - ra - hiny - er - a Ghati omote*
Robhi kba - nj - mz - utd - kbt Ghati mti

Robhi anamwinamishia Ghati mti

(34). *Robhi na Ghati bha - ra - hiny - er - an - a omote*
Robhi na Ghati kba - nj - mz - utd- utn - kbt mti
Robhi na Ghati wanainamishiana mti

(35). *Anna na Mwita bha - hanch - er - an - a ichimbiria*
Anna na Mwita kba - mz - utd - utn - kbt pesa
Anna na Mwita wanapendeana pesa

b. *Anna na Mwita bha - hanch - an - er - a ichimbiria*
Anna na Mwita kba - mz - utn - utd - kbt pesa
Anna na Mwita wanapendania pesa

Tukiangalia jinsi yambwa zinavyozalishwa katika lugha hii kwa njia ya unyambulishaji, tunaona kuwa, kuwapo kwa kauli ya utendea kumelazimisha yambwa kuwapo kama hitaji mojawapo la kitenzi hiki. Halikadhalika, viambishi vya utendano vimefanya mabadiliko ya yambwa *Ghati* kuhamia kwenye nafasi ya mtenda na kuwa na hadhi sawa na mtenda *Robhi* na wakati huohuo wote wawili kuwa watendwa. Viambishi hivi pia vimeweza kubadilishana nafasi na kuathiri maana ya kitenzi.

### 4.1.3 Kauli ya Usababishi na Utendwa

Lugha hii pia inaruhusu muunganiko wa kauli ya usababishi na utendwa kama inavyooneshwa katika sentensi zifuatazo:

(36)a. *omoona a - ra - mbuk - a omoro*
mtoto kba - nj - mz - kbt mto
mtoto anavuka mto

b. *omoona a - ra - mbuk - i - bhw - a omoro na nyakwabho*
mtoto kba - nj - mz - usb - utw na mama yake
mtoto anavushwa mto na mama yake

c. *omoona a - ra - mbuk - i - bhw - a omoro*
mtoto kba - nj - mz - usb - utw
mtoto anavushwa mto

(37)a. *Mkami a - ra - bhín - i - bhw - a ilibhina na omorokya*
Mkami kba - nj - mz - usb - utw - kbt wimbo na mwalimu
Mkami anaimbishwa wimbo na mwalimu

b. *Mkami a - ra - bhín - i - bhw - a ilibhina*
Mkami kba - nj - mz - usb - utw - kbt wimbo
Mkami anaimbishwa wimbo

(38)a. *umwiseke a - ra - tah - a amanche*
msichana kba - nj - mz - kbt maji
msichana anachota maji

b. *umukungu a - ra - tah - i - a umwiseke amanche*
mama kba - nj - mz - usb - kbt msichana maji
mama anamchotesha msichana maji

c. *umwiseke a - ra - tah - i - bhw - a amanche na umukungu*
msichana kba - nj - mz - usb - utw - kbt maji na mama
msichana anachoteshwa maji na mama

d. *umwiseke a - ra - tah - i - bhw - a amanche*
msichana kba - nj - mz - usb - utw - kbt maji
msichana anachoteshwa maji

Muungano wa kauli ya usababishi na utendwa hulazimisha kipashio kilichoongezwa na usababishi kuwekwa mwishoni mwa sentensi badala ya kuwa mwanzoni mwa sentensi kama ilivyo kawaida ya kauli hii. Wakati huohuo kauli ya utendwa hukiondoa kipashio hicho kwa sababu si cha lazima na hatimaye kitenzi hiki hubaki na kipashio cha lazima kimoja tu kulingana na uhitaji wa kitenzi. Mabadiliko haya yanasababishwa na kauli ya utendwa ambayo yambwa ni lazima ichukue nafasi ya mtenda ijapokuwa itabaki kuwa na dhima yake ileile ya utendwa.

## 4.2 Muunganiko wa Kauli tatu katika Kitenzi kimoja

Lugha hii inakubali kuambikwa kauli tatu kwa wakati mmoja katika kitenzi kimoja. Kama inavyojidhihirisha hapa chini:

### 4.2.1 Muunganiko wa Usababishi, Utendea na Utendano

Kikuria kinaruhusu muunganiko wa kauli tatu. Mifano ifuatayo inaonesha muunganiko wa kauli za usababishi, utendea na utendano. Hii inaonesha kuwa Kikuria kinakubaliana na pendekezo la Hyman (2003) kwamba mfuatano wa kauli katika lugha za Kibantu huweza kuwekwa pamoja katika kitenzi kimoja. Mfano, kauli ya usababishi > utendea > utendano (CAR). Kwa upande mwingine Lugha hii inapingana na Hyman (2003) kwa kuruhusu mpishano huru. Mfano: ACR, ARC, RAC, RCA na CRA[5] na mfuatano huru huu huathiri maana ya

[5] CRA : C- Causative (usababishi) , R- Reciprocal (utendano), na A- Applicative (utendano)

kitenzi. Mifano ifuatayo inaonesha jinsi gani kauli hizi zinavyoweza kubadilishana nafasi na athari zake kisintaksia na maana.

(39). *abhaana bha - ra - h - er - an - i-a Mwita omoona umubhiira kebhara*
abhaana kba - nj - mz - utd - utn - usb - kbt Mwita child ball outside
watoto wanampa mtoto mpira nje kwa niaba ya Mwita.

c. *Mbusiro na Ghirimwa bha - ∅ - h - an -ir - i - a nyakwabho ichimbiriya*
Mbusiro na Ghirimwa kba - nj - mz - utn - utd- usb - kbt mama fedha
Mbusiro na Ghirimwa wamemlipia mama yao fedha.

Matokeo ya kuweka pamoja viambishi nyumbulishi hivi kila kimoja hutenda kazi yake sawa sawa, *Ghati* na *omoona* wamewekwa pamoja kutokana na utendano lakini wakati huohuo kila mmoja ni msababishi wa mwingine na utendea umelazimisha kuwapo kwa kipashio kingine (33)a '*ebhite*' (yambwa). Katika mifano hii 33 a-c unaweza kuona jinsi lugha hii inavyopingana na mfuatano wa Hyman (2003).

### 4.2.2 Muunganiko wa Utendeka, Utendwa na Utendano

Mifano ifuatayo inaonesha muunganiko wa utendeka, utendwa na utendano. Hii inadhihirisha kuwa Kikuria hakifungwi katika mfuatano wa aina moja kama pendekezo la Hyman (2003), kwa sababu Hyman hakushughulikia kauli ya utendeka hivyo basi mfuatano wa kauli hizi katika lugha hii umekuwa tofauti na lugha nyingine za Kibantu, yaani kauli utendeka > utendwa > utendano.

(40) *emete ghé - bhon- ek - ér - an - a kunguku*
miti kba - mz - utk - utd - utn - kbt mlimani
miti imevunjikiana mlimani

(41) *ibhinto bhi - at - ek - ér - an - a ghokabhati*
vyombo kba - mz - utk - utd - utn - kbt kabatini
vyombo vimevunjikiana kabatini

### 4.2.3 Muunganiko wa Utendano, Usababishi na Utendwa

Pia tunaona kuwa Kikuria kinaruhusu kauli ya utendano - usababishi - utendwa kama ifuatavyo:

(42) *Mwita na Robi bha - hánch - an - i - bhw - a na abhaibhuri*
Mwita na Robi kba - mz - utn - usb - utw - kbt na wazazi
Mwita na Robi wamependanishwa na wazazi

Hivyo basi, lugha hii imekuwa miongoni mwa lugha za Kibantu ambazo zinakubali kuambikwa kauli tatu kwa wakati mmoja. Athari inayojitokeza hapa ni kuwa kila kauli hutenda kazi yake kama kawaida. Mfano (42) '*Mwita na Robi'* ni vipashio vyenye dhima ya mtenda lakini wakati huo huo ni watendeshwa wa msababishi *abhaibhuri* 'wazazi'.

### 4.3 Muunganiko wa Kauli nne katika Kitenzi kimoja

Baadhi ya viambishi katika lugha ya Kikuria vinapoungana huonesha matendo mfuatano. Haya yanajidhihirisha katika vipengele vifuatavyo.

#### 4.3.1 Muunganiko wa Kauli ya Utendea, Utendano, Usababishi na Utendwa

Lugha hii ni mojawapo ya lugha za Kibantu ambayo vitenzi vyake huweza kuambikwa mwingiliano wa kauli hadi nne katika kitenzi kimoja. Muunganiko huo waweza kuwa kauli ya utendea - utendano - usababishi - utendwa. Mifano:

(43) a. *Mwita na Mary bha - ra - sóm - er - an - i - a abhaana*
Mwita na Mary kba - nj - mz - utd - utn - usb - kbt watoto
Mwita na Mary wanawasomea watoto wakati wanasomeana

b. *abhaana bha - ra - sóm - er - an - i - bhw - a Mwita na Mary*
watoto kba - nj - mz - utd - utn - usb - utw - kbt Mwita na Mary
watoto wanasomewa na Mwita na Mary wakati wao wanaposomeana

(44). *ibhinto bhyane bhi - a - bhek - er - an - i - bhw - a nibhyao*
vitu vyangu kba - nj - mz - utd - utn - usb - utw - kbt na vyako
vitu vyangu vimetunzwa pamoja na vyako au wakati wanatunza vitu vyako walitunza na vya kwangu aidha kwa kujua ama kutokujua.

Mwita na Mary wanasomeana na wakati huohuo wanawasomea watoto. Muungano wa kauli hizi husababisha kitenzi kionekane kama vitenzi viwili vinavyokwenda sambamba. Mfano, katika (43)b, inaonekana kuwa *Mwita* na *Mary* wanasomeana lakini wakati huohuo wanafanya kazi ya kuwasomea watoto. Kitenzi *bheka* 'tunza' katika na. 38 kinaeleza kuwa wakati wanatunza vitu vya mtu mmoja pia walikuwa wanatunza pamoja na vya mtu mwingine (vyangu).

#### 4.3.2 Muunganiko wa Kauli ya Usababishi, Utendea, Utendano na Usababishi

Pia tunaona muunganiko wa kauli ya usababishi, utendea, utendano na usababishi kama inavyooneshwa katika mifano hii:

(45). *abhaana bha - ra - síngís - i - er - an - i - a abhakungu ichinchubha*
watoto kba - nj - mz - usb - utd -utd - usb - kbt wanawake chupa watoto
wanatingishiana chupa na wakati huohuo watoto wanawatingishia wanawake chupa

(46). *abhakungu bha - ra -tem- er - an - i - bhw - a na abhaana*
akinamama kba -nj -mz - utd - utn - usb - utw - kbt na watoto
akinamama wanapigwa pamoja na watoto au wakati watoto wanapigwa
akinamama wamepigwa ndani ya kundi hilo aidha kwa kujua au kwa kutokujua

Mifano hii inadhihirisha wazi jinsi kauli hizi zinavyoweza kufungamanishwa katika kitenzi kimoja na kuleta athari kisintaksia kwa kueleza dhana mbili kwa wakati mmoja na wakati mwingine kuonekana kama vitenzi viwili vilivyoshikana vinavyofanyika sambamba.

Muunganiko wa kauli hizi huruhusu kauli mojawapo kujirudia baada ya mwingiliano wa kauli zingine katikati (mfano 45). Kauli ya usababishi inaonekana kujitokeza kwa mara ya pili baada ya utendea na utendano.

## 5.0 Hitimisho

Makala haya yamejaribu kuonesha unyambulishaji katika lugha ya Kikuria kwa kutumia vitenzi mbalimbali na vyenye sifa tofauti. Pia, yamebaini kuwa mofu za unyambulishaji huweza kuleta athari kisintaksia kama inavyojidhihirisha hapo juu. Mofu za kauli za utendea na usababishi huathiri kitenzi si tu elekezi kuwa elekezi bali pia kitenzi elekezi kuhitaji kipashio kingine ili kukamilisha maana iliyokusudiwa. Kukosekana kwa kipashio hicho hukifanya kitenzi hicho kutokukubalika kisarufi. Wakati kauli ya utendano, utendwa na utendeka hukiondolea kitenzi uwezo wa kuhitaji yambwa au kipashio kingine huleta mabadiliko ya dhima baina ya vipashio vya sentensi. Pia hukifanya kitenzi kiwe na uhiari wa kuwekewa baadhi ya vipashio au kutokuwekwa. Makala haya pia yamebaini kuwa vitenzi vya Kikuria huweza kuambikwa viambishi vinyambulishaji vya kauli hadi vinne kwa wakati mmoja, tofauti na lugha ya nyingine za Kibantu ambazo idadi ya viambishi huwa ni tatu (Rugemalira 1993, 2005). Kuambikwa kwa viambishi vinne huleta athari ya kitenzi kuonekana kuwa kuna vitenzi viwili vilivyogandiana ambavyo hufanyika sambamba katika tendo lile lile na kuathiri wahusika wengine ambao hawakuwamo ama kwa bahati mbaya au kwa makusudi. Fauka ya hayo yote, lugha hii imejidhihirisha kuwa inaruhusu pia mfuatano huru ambao ni kinyume na mfuatano wa Hyman (2003).

## Marejeo

Eastman, C.M. (1967). 'An Investigation of verbal Extension in Kenya Costal Dialects of Swahili with Special Emphasis on Kimvita', Unpublished Ph.D Linguistics Thesis, University of Wisconsin.

Ezekiel, P. (2007). 'Verb Extensions in Giha and Constraints on Ordering and Co-occurrence'. Tasnifu ya Uzamili (Haijachapwa), Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Guthrie, M. (1970). "The Status of Radical Extensions in Bantu Languages", in M. Guthrie, *Collected Papers on Bantu Linguistics,* Farnborough, Gregg International Publishers (Original Work Published 1962), pp. 99-110.

Hyman, L.M. (2003). 'Suffix ordering in Bantu: A morphocentric approach'. in Booij, Geert & Marle, Jaap van (eds.). *Yearbook of Morphology*. Dordrecht: Kluwer Academic. pp. 245-281.

Kaoneka, S. (2009). 'Verb Extension in Shambala: Their Occurrence and Co-occurrence Constraints'. Tasnifu ya Uzamili (Haijachapwa) Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Khamis, A.M. (2008). *Maendeleo ya Uhusika*. Dar es Salaam: Institute of Kiswahili Studies.

Khamisi, A. M. (1985). 'Swahili Verb Derivation', Unpublished PhD Linguistics Thesis, Hawaii University.

Kihore, Y., D.P.B. Massamba & Y. Msanjila (2003). *Sarufi Maumbo ya Kiswahili Sanifu: Sekondari na Vyuo.* Dar es Salaam: Institute of Kiswahili Research.

Lodhi, A.Y. (2002). 'Verbal Extension in Bantu: The Case of Swahili and Nyamwezi' *Africa and Asia: Goteborg Working Papers on Asian and African Languages and Literatures,* Vol. 2 pp. 4-26.

Massamba, D.P.B. (2004). *Kamusi ya Isimu na Falsafa ya Lugha*. Dar es Salaam: Institute of Kiswahili Research.

Masebo, H. (2007). 'The Verb Extension in Chindali'. Tasnifu ya Uzamili (Haijachapwa) Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Meinhof, C. (1932). *Introduction to the Phonology of the Bantu Languages* Translated by N. J. Van Warmelo (ed). Berlin: Dietrich Reimer Verlag.

Moore, R. A. C. (1966). 'Verbal Derivations in Swahili', Unpublished PhD Linguistics Thesis, University of Texas.

Mreta, A.Y. (1998). *An Analysis of Tense and Aspect in Chasu: Their Forms and Meaning in the Affimative Constructions*. Hamburg: LIT.

Muhdhar, R. (2006). 'Verb Extensions in Kisukuma- Jinakiiya Dialect'. Tasnifu ya Uzamili (Haijachapwa) Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Mushi, C. P (2005). 'Verb Derivation in Kibosho'. Tasnifu ya Uzamili (Haijachapwa) Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Rugemalira, J. M (2005). 'A Grammar of Runyambo', *Occasional Papers in Linguistics* No.1. Dar es Salaam, Languages of Tanzania Project, University of Dar es Salaam.

______(1993). Runyambo Verb Extensions and Constraints on Predicate Structure, Unpublished Ph.D Linguistics Thesis, University of California, Berkeley.

Zacharia, M. (2011). 'Verb Extensions in Kuria: Co-occurrence and ordering Restrictions'. Tasnifu ya Uzamili (Haijachapwa) Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.